



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII



CHUO CHA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI
MWEKA

MAFUNZO YA MUDA MFUPI KWA WAONGOZA WATALII

Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka itaendesha mafunzo kwa waongoza watalii ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma bora katika sekta ya Utalii. Gharama za mafunzo, chakula na shajara zimefadhiwa kupitia mpango wa mandeleo na ustawi wa Taifa wa mapambano dhidi ya Uviko-19. Walengwa ni waongoza watalii wenye leseni na waliosajiliwa na Wizara. Mafunzo yanatarajiwa kuanza tarehe 10/01/2022 hadi tarehe 02/04/2022 kwa awamu kama ilivyoainishwa kwenye jedwali lifuatalo:

Tarehe	Kanda	Kituo cha Mafunzo
10 Januari – 22 Januari, 2022	Kanda ya Arusha, Singida, Kilimanjaro na Manyara	Eneo la mafunzo Chuo cha Mweka - Kwakuchinja
24 Januari – 5 Februari, 2022	Kanda ya Dar es salaam, Morogoro, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara	Hifadhi ya Taifa Saadani
7 Februari – 19 Februari, 2022	Kanda ya Mbeya, Rukwa, Songwe na Katavi	Mt Rungwe Nature Reserve-TFS Mbeya
21 Februari – 5 Machi, 2022	Kanda ya Kusini Iringa, Njombe, Dodoma na Ruvuma	Hifadhi ya Taifa Ruaha
7 Machi – 19 Machi, 2022	Kanda ya Mwanza, Kigoma, Tabora, Simiyu, Mara, Geita na Kagera	Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato
21 Machi - 2 Aprili, 2022	Kanda ya Arusha, Singida, Kilimanjaro na Manyara	Eneo la mafunzo Chuo cha Mweka - Kwakuchinja

Washiriki wanatakiwa kujiandikisha kwenye mfumo kupitia kiunganishi

<https://smis.mwekawildlife.ac.tz/shortcourse.php> kabla ya tarehe 31/12/2021. Washiriki

wanatakiwa kuja na mahema yao kwa ajili ya malazi wakati wa mafunzo.

TAFADHALI ZINGATIA TAREHE NA VITUO VYA MAFUNZO UPATAPO TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZIO

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na
Dkt Gabriel Mayengo 0767465668
Vitales Kabonda 0654369818
10/12/2021